

## HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA



### TANGAZO LA ZABUNI YA UWAKALA WA UKUSANYAJI WA MAPATO KATIKA MWALO WA KIJIWENI HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA KWA MWAKA WA FEDHA 2021-2022

ZABUNI NA. LGA/094/HQ/NCS/2021-2022/03

Tarehe 28/06/2021

Halmashauri ya wilaya ya Sengerema inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kukusanya ushuru/mapato/ ada mbalimbali katika Mwalo wa Kijiweni Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.

#### Maombi yote ya Zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-

- a) Nyaraka za zabuni kwa lugha ya Kiswahili zinapatikana kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni baada ya kulipia ada ya maombi ya Tsh. 100,000.00 baada ya kupata namba ya malipo (Control Number) kutoka ofisi ya mapato iliyopo Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema
- b) Ombi la Zabuni liwe na jina na anuani halisi ya mwombaji, aidha aonyeshe mahali ofisi zake zilipo au anapoweza kupatikana (Physical Address).
- c) Muombaji ambae ana uzoefu katika ukusanyaji wa mapato atapewa kipaumbele.
- d) Mkataba utakuwa wa miezi kumi na moja (11) kuanzia tarehe 1/08/2021 hadi 30/06/2022
- e) Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (Power of Attorney) wa mtu anayehusika na zabuni hii
- f) Muombaji hatakiwi kuwa mtumishi au kiongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.
- g) Muombaji aonyeshe Mchanganuo wa Maoteo ya Mapato anayotarajia kukusanya, matumizi anayotarajia kuyafanya na kiasi cha asimilia atakacholipwa na Halmashauri kwa mwezi.
- h) Zingatia kuwa fomu ya maombi ya Zabuni inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (Power of Attorney) katika zabuni hii, kama ni kampuni.
- i) Muombaji aambatishe nakala ya Leseni ya biashara husika (leseni ya uwakala) kama ipo.
- j) Muombaji aambatanishe nakala ya uthibitisho wa ulipa kodi (Tax Clearance) kama ipo.
- k) Muombaji aambatanishe nakala ya VAT/TIN

1) Muombaji wa zabuni endapo atachaguliwa atahitajika kuleta dhamana ya kufanya kazi kwa njia ya fedha taslimu (Cash Bond) malipo ya miezi miwili kiasi kitakachokuwa katika makubaliano baina ya Mzabuni na Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema (Hii ni kwa wazabuni watakao shinda zabuni). Mzabuni hataruhusiwa kusaini mkataba kabla ya kuwasilisha dhamana hiyo.

1. Muombaji aoneshe vifaa alivyonavyo, idadi ya wafanyakazi na uzoefu wao.
2. Muombaji awasilishe zabuni halisi (Orginal) na nakala mbili (2) endapo maelezo ya Zabuni halisi na nakala yatatofautiana, zabuni halisi ndio itatumika kwenye tathmini.
3. Zabuni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha isiyo na maandishi yoyote (Plain) na juu ya bahasha iandikwe, namba ya zabuni, kazi inayoombwa, 'Original' au 'Copy'.
4. Uongozi haulazimiki kumchagua mzabuni yoyote. Aidha wazabuni au watoa huduma wote ambao walipewa zabuni miaka iliyopita na wakashindwa kutekeleza matakwa ya mkataba ikalazimu uvunjaji wa mkataba kati ya Halmashauri na Mzabuni/mtoa huduma, hawaruhusiwi kuomba zabuni.
5. Mwisho wa kupokea zabuni ni **saa Tano (5) kamili asubuhi** (saa za Afrika Mashariki) ya tarehe **19/07/2021** siku ya **Jumatatu** katika **Ofisi ya Katibu wa bodi ya zabuni (Ugavi)** zilizopo **Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema**. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo utakaofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri.
6. Kwa wafanyabiashara/Makampuni/Vikundi/Ushirika ambao watapenda kuomba Zabuni hiyo wafike katika ofisi ya **KATIBU WA BODI YA ZABUNI** ya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kwa ajili ya;
  - Maelezo zaidi yanayohusu Zabuni hii
  - Kununua kabrasha la Zabuni ambalo linauzwa Tsh.100,000.00 fedha ambazo hazitarudishwa na kabla ya kulipa utatakiwa kufika ofisi ya mapato iliyopo Halmashauri kuchukua namba ya malipo (Control namba)
  - Kupata nyongeza (Addition/Ammendment) ya kabrasha la Zabuni kama litakuwepo.
7. Anuani ya kutuma zabuni ni:-

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA,  
S.L.P. 175, SENGEREMA.**
8. Mzabuni/ mwakilishi yeyote atakayehudhuria ufunguzi lazima awe amechukua tahadhari ili kujikinga na maambukizi ya 'COVID 19, endapo Mzabuni/Mwakilishi Atakuwa Hajachukua tahadhari hataruhusiwa kuingia ndani ya Ukumbi wa Ufunguzi, na hii inawahusu wote watakaokuwa wanahusika wakati wa ufunguzi wa kabrasha la zabuni.
9. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa mtandao (e-mail) hazitashughulikiwa.

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
SENGEREMA**